MKATABA WA HUDUMA

HALMSHAURI YA HAKIMILIKI YA KENYA

KULINDA HAKIMILIKI NA KUKUZA UBUNIFU

HALMSHAURI YA HAKIMILIKI YA KENYA

MKATABA WA HUDUMA

Utangulizi

Halmashauri ya Hakimiliki ya Kenya (KECOBO) ni shirika la serikali lililoundwa kutokana na Ibara ya 3 ya Sheria ya Hakimiliki sura ya 130 ya Sheria za Kenya, ili kusimamia na kutekeleza hakimiliki pamoja na haki nyinginezo zinazohusiana nayo.

Halmshauri ya Hakimiliki ya Kenya imeandaa mwongozo huu ili kuwasiliana na kuthibitinishia wateja wake wa ndani na nje kujitolea kwa halmashauri hii kutoa huduma bora. Mwongozo huu unaratibu majukumu ya KECOBO, sera ya ubora, maazimio, dhamira na huduma zake mbalimbali.

Majukumu ya Halmshauri ya Hakimiliki ya Kenya

Katika kutimiza wajibu wake wa kusimamia na kutekeleza hakimiliki na haki zinazohusiana nayo, Halmshauri ya Hakimiliki ya Kenya itafanya yafuatayo;

1. Kutekeleza, kuratibu, na kusimamia utekelezaji wa sheria na mikataba ya kimataifa na maazimio ambayo Kenya imetia saini na yanayohusiana na hakimiliki na haki nyinginezo zinazotambuliwa na Sheria hii na kuhakikisha uzingatiaji wa sheria hii.
2. Kutoa leseni na kusimamia shughuli za mashirika ya umoja wa wasanii/wadau kulingana na sheria.
3. Kubuni na kutekeleza programu za mafunzo kuhusu hakimiliki na haki nyinginezo zinazohusiana nayo.
4. Kufanyia marekebisho ya mara kwa mara sheria ya hakimiliki na sheria nyinginezo zinazohusiana nayo.
5. Kuhamisisha na kufahamisha umma kuhusu masuala yanayoambatana na hakimiliki na haki nyinginezo zinazohusiana nayo.
6. Kuhifadhi mfumo wa maelezo na takwimu kuhusu waandishi na kazi zao; kusimamia masuala yote ya hakimiliki na haki nyingine zinazohusiana Sheria hii; na kushughulikia masuala ya msaada na majukumu yake kulingana na sheria hii.
7. Kuhakikisha kulindwa kwa maarifa ya jadi na mambo ya kitamaduni.

Sera ya Ubora

Halmshauri ya Hakimiliki ya Kenya (KECOBO) imejitolea kuhudumu na kulinda mfumo bora wa usimamizi kwa mujibu wa matakwa ya viwango vya kimataifa vya ISO 9001:2008.

Ruwaza

Kuwa asasi ya viwango vya kimataifa ya utekelezaji wa hakimiliki nausimamizi wa maarifa ya jadi.

Dhima

Kuendeleza ukuzaji wa tasnia za kibunifu kwa kusimamia na kutekeleza hakimiliki ili kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi nchini Kenya.

Kanuni Zetu na Nguzu Zetu za Maadili

- **Utimilifu wa kitaalamu na viwango vya maadili**- tutajiendesha kwa utimilifu na kwa kudumisha viwango vya juu vya utaalamu na maadili.
- **Kujitolea**- tutajitolea kupata matokeo bora na kutimiza majukumu yetu kwa mafanikio makubwa.
- **Uwajibikaji na uwazi**-tutadumisha viwango vya juu vya uwajibikaji na uwazi katika utendaji wetu.
- **Utendakazi**: tutatimiza wajibu wetu kwa mafanikio, kutoa huduma bora na kuwajibikia mahitaji ya wadau wetu wote.
- **Heshima na utangamano**- tutadumisha heshima na utangamano mwema na kuepuka ubaguzi kwa msingi wa jinsia, rangi au dini.

Ahadi Yetu katika Kuafikia Ruwaza ya Mwaka 2030

Halmshauri ya Hakimiliki ya Kenya itahakikisha utekelezaji kamili wa sheria ya Hakimiliki kwa lengo la kukuza ubunifu na kuzalisha mali na kubuni nafasi za ajira.

Wadau wetu

- Waasisi wa kazi za kubuni kama vile waandishi wa vitabu, wasanii wa uchoraji.
- Waandalizi/maprodusa wa kazi za kubuni.
- Serikali.
- Mashirika yaliyomo katika sekta hii.
- Mashirika ya umoja wa wasanii.
- Vyombo vya habari.
- Shule, vyuo vya kati na mashirika ya utafiti.
- Watumiaji wa kazi zenye hakimiliki.
- Wahifadhi wa maarifa ya jadi na mambo ya kitamaduni.
- Maafisa wa utekelezaji wa sheria.

Viwango vya Ubora wa Huduma Zetu

Tumejitolea:

- Kukushughulikia na kukuelekeza kwenye vituo vifaavyo vya huduma unapokuja katika ofisi zetu.
- Kujibu barua yako katika muda wa siku 7 baada ya kuipokea.
- Kushughulikia matatizo yako ifaavyo kwa faragha na haraka.

HUDUMA	UNACHOHITAJI	GHARAMA	MUDA
Usajili/uandikishaji wa kazi ya hakimiliki	• Fomu mbili za usajili zilizojazwa na kutiwa saini na wakili. • Nakala mbili maalum za kazi ya kusajiliwa. • Barua ya idhini iwapo mwasisi wa kazi hiyo hayupo.	Ksh. 1,000/= kwa kila kazi	Siku saba za kufanya kazi
Kifaa cha kukabiliana na kughushi kazi za hakimiliki (APSD).	• Ithibati ya usajili wa hakimiliki. • Fomu zilizojazwa za kuthibitisha uhalali wa kazi ya hakimiliki. • Barua ya idhini iwapo mwasisi wa kazi hiyo hayupo.	Ksh. 4/= kwa kila kifaa cha APSD na kibandiko cha msimbo pau (bar code sticker).	Siku 3 za kufanya kazi
Mashtaka ya Ukiukaji wa hakimiliki.	• Malalamiko na uthibitisho wa umiliki wa hakimiliki	Hakuna malipo	Muda ufaao
Ushauri wa kisheria	• Upangaji miadi/mkutano na wakili	Hakuna malipo	Kati ya siku 14 na 21

HUDUMA	UNACHOHITAJI	GHARAMA	MUDA
Upatanishi katika mizozo ya hakimiliki	• Nakala za kazi za awali na zilizoghushiwa • Stakabadhi za kuthibitisha • Kibali cha pande zote kutaka kupatanishwa	Hakuna malipo	Muda ufaao
Mafunzo ya wamiliki wa hakimiliki	• Barua ya maombi • Angalao arifa ya wiki mbili	Hakuna Malipo	Kuthibitishwa mafunzo katika muda wa siku 7 baada ya kupokea ombi la mafunzo. Muda wa mafunzo ni kati ya nusu siku na siku nzima.

HUDUMA	UNACHOHITAJI	GHARAMA	MUDA
Kutoa leseni kwa mashirika ya umoja wa wasanii	• Nakala iliyothibishwa ya cheti cha usajili. • Nakala iliyothibitishwa ya cheti au makubaliano ya ushirikiano. • Nakala zilizothibitishwa za mapato ya kila mwaka pale ambapo pana mapato. • Iwapo umoja wa wasanii umesajiliwa hivi karibuni, hesabu za fedha au mapato yaliyokaguliwa katika mwaka uliotangulia ule wa maombi ya usajili. • Ripoti ya shughuli za umoja huo ya mwaka unaotangulia ule wa maombi ya usajili. • Mwafaka wa wajibu wa haki kwa kila mwanachama. • Uwezo wa kukusanya na kusambaza mapato/ Mirabaha	Ksh.250,000/=	Katika muda wa miezi mitatu. **Tanbihi**: *Ombi la kutaka leseni linapaswa kuwasilisha miezi mitatu kabla kumaliza kwa muda wa leseni hiyo.*

Majukumu ya Wadau / Wateja Wetu

- Kuipa Halmashauri ya Hakimiliki ya Kenya habari za kweli na kwa wakati ufaao ili hatua yoyote ichukuliwe.
- Kuwasilisha kila kitu kitakiwacho ili kusajiliwa kwa kazi ya hakimiliki na usimamizi wa vifaa vya kukabiliana na kughushiwa kwa kazi ya hakimiliki (Anti-Piracy Security Device (APSD).
- Kutoa habari kuhusu kisa chochote cha ufisadi au ukiukaji wa maadili ya kitaalamu kinachomhusisha mfanyikazi wetu yeyote.
- Kudumisha ustaarabu na maadili ya kitaalamu na kujiepusha na tabia isiyofaa na kuwapotosha au kuwatisha maafisa wa KECOBO.

Malalamiko

Halmashauri ya Hakimiliki ya Kenya inachukulia malalamiko kuwa njia mwafaka ya kuboresha huduma. Endapo una malalamiko yoyote kuhusu mfanyikazi wa KECOBO au viwango vya ubora wa huduma zetu tafadhali tufahamishe kuhusu malalamiko hayo kwa njia ya baruapepe, simu, visanduku vya maoni na fomu za maoni ya wateja zinazopatikana katika ofisi zetu. Uongozi unaahidi kushughulikia malalamiko hayo haraka iwezekanavyo na ifaavyo. Halmashauri ya Hakimiliki ya Kenya inatoa hakikisho kwamba faragha na usiri vitadumishwa katika mawasiliano yote.

Kuwasiliana Nasi

Halmashauri ya Hakimiliki ya Kenya

Orofa ya tano Jengo la NHIF-Community

Barabara ya Ragati,

S.L.P 34670 - 00100

Nairobi.

Simu +254 – 020 - 2533869/59

Rununu: 0713 – 761 758

Baruapepe: info@copyright.go.ke

Tovuti: www.copyright.go.ke

Twitter: @KenyaCopyright

Facebook: Kenya Copyright Board

Complaints: corruption@copyright.go.ke,
complaints@copyight.go.ke,

In support of Vision 2030